

HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu Na. 027-2531011/55

Fax Na. 027-25311055

Email: info@babatidc.go.tz
ded@babatidc.go.tz



S.L.P. 400,
BABATI.

06.05.2018

TANGAZO LA MNADA


Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati anawatangazia Wananchi wote kuwa, kutakuwa na mnada wa hadhara wa kuuza mali chakavu za Halmashauri ya Wilaya Babati utakaofanyika eneo la Mrara katika yadi ya Ujenzi siku ya Jumamosi tarehe 19/05/2018 kuanzia saa 4:00 asubuhi. Orodha ya mali hizo zimeainishwa katika jedwali hapa chini

S/N	LOT NO	Namba ya usajili	Aina ya gari	Hali ya gari
1	LOT 1: DC/BBT/2017	STK 804	MITSUBISH L-200 Double cabin P/U	Halitumiki
2	LOT 2: DC/BBT/2017	STK 323	ISUZU Double Cabini TDI 300 KB 4X4 P/UP	Halitumiki
3	LOT 3: DC/BBT/2017	STK 5165	TOYOTA V8 D-4D	Halitumiki
4	LOT 4: DC/BBT/2017	STG 9123	MITSUBISHI L-200 S/Cabin P/UP	Halitumiki

MASHARTI YA MNADA

1. Mnunuzi atakaye fika bei ya juu kuliko wote ndiye atakayekuwa mnunuzi halali katika mnada huo na atatakiwa kulipa 25% ya bei aliyofikia baada ya nyundo ya dalali kuangushwa, na atamalizia salio la 75% ndani ya siku 14 baada ya mnada. Mnunuzi atakayeshindwa kulipa 75% ndani siku 14, ushindi wake utafutwa na hatarudishiwa kiasi alichotanguliza, na mali hiyo itanadiwa tena
2. Ukaguzi wa magari utafanyika siku tatu kabla ya mnada kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 7:00 mchana
3. Magari yanauzwa jinsi yalivyo na kama yanavyoonekana
4. Ikumbukwe kuwa magari yanayouzwa hayajalipiwa kodi na malipo mengine hivyo ni wajibu wa mnunuzi kulipa kodi na malipo kwa serikali

5. Mnada utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 19/05/2018 kuanzia saa 4:00 asubuhi
6. Walio na nia ya kushiriki mnada watatakiwa kulipia malipo ya Tsh 50,000, fedha hizo zitapokelewa Ofisi ya uhasibu Halmashauri ya Wilaya Babati na fedha hizo hazitarudishwa, siku ya mnada mshiriki aje na risiti kuonesha ushiriki.
7. Kwa mawasiliano zaidi, wasiliana na Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Babati, P.O Box 400, Babati-Manyara



Hamisi Iddi Malinga
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA BABATI

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI